

Virusi vya korona – mabadiliko ya utendakazi wa manispaa ya Vihti

24.3.2020

Serikali ya Ufini ilibaini tarehe 16. mwezi wa sita 2020, kwamba nchi iko katika hali ya dharura kutokana na maambukizi ya virusi vya korona. Serikali ilitangaza sera za harakati za ziada kwa kushughulikia hali ya virusi vya korona nchini. Lengo la harakati hizo ni kuwalinda watu pamoja na kuhakikisha amani kwenye jamii na uchumi kufanya kazi. **Sera zilizotangazwa sasa zitaendelea kufanya kazi mnamo 18.3.-13.4.2020.**

Kwa mujibu wa sera za serikali, katika manispaa ya Vihti:

- **Mashule yatafungwa na masomo ya kuhudhuria yatasimamishwa. Badala ya masomo ya kuhudhuria, mafunzo na uongozo utatolewa kwa njia ya masomo ya mbali.** Mwanzoni mwa hali ya dharura kutokana na virusi vya korona masomo ya kuhudhuria yalipatiwa kwa wanafunzi ambao wazazi wao wanafanya kazi kwenye sekta nyeti za jamii. Ijumaa tarehe 20.3. serikali ilibadilisha sera yake, na kwa sasa hivi wanafunzi wote wa elimu ya msingi wa darasa la 1-3 wanaweza kupatiwa masomo ya kuhudhuria *panapohitajika*. Lakini waziri wa elimu alitoa wito kwa wazazi, kwamba wasiwatume watoto shuleni, kama si lazima. Maelekezo zaidi yatatumwa kupitia Wilma.
- **Chekechea na elimu ya awali** itapatiwa kwa watoto ambao wazazi wao wanafanya kazi kwenye sekta nyeti za jamii. Inapendekezwa mtoto atunzwe nyumbani, kama uwezekano huo upo.
- **Kumbi za vijana** hazifanyi kazi.
- **Maktaba, magari ya maktaba na majumba ya makumbusho** yamefungwa.
- **Ukumbi wa kuogelea na chumba cha mazoezi** kimefungwa. Vikundi vya mafunzo ya mazoezi vya manispaa vya ardhi kavu na vya maji vimesimamishwa.
- **Huduma za makao makuu ya manispaa** zitatolewa kupitia simu, kielektroniki au kwa kupangiwa muda.

Pia kwa mujibu wa sera za serikali:

- Imedhibitiwa watu zaidi ya 10 hawapaswi kukusanyika katika sehemu za umma. Inapendekezwa watu wasikae sehemu za umma bila sababu maalum.
- Ni marufuku kutembelea senta za makao ya wazee na watu wengine walio miongoni mwa makundi ya watu wenye hatari kubwa.
- Ni marufuku kwa wageni kutembelea mahospitali, vitengo vya matunzo na vituo vya afya. Kulingana na hali, makadirio yenye vigezo vikali yatafanyika kuhusu safari za ndugu wasio na dalili za ugonjwa kuwatembelea wagonjwa mahututi na watoto, pamoja na wale wanaopatiwa huduma za tiba shufaa, na mwenzi au mtu wa kuunga mkono kuwepo kwenye kitengo cha kujifungua.
- Watu walio na miaka zaidi ya 70 wanashauriwa kuepukana na kushirikiana na watu wengine, inavyowezekana tu kulingana na hali halisi, (mazingira yanayofanana na karantini). Hayo hayawahusu wabunge, viongozi wa serikali na wenye mamlaka wa manispaa.
- Waajiri wa sekta za umma wataamuru wafanyakazi wa sekta ya umma kufanya kazi kwa njia ya kazi ya mbali, kama itawezekana kulingana na kazi zao.
- Wafini na wenye makazi ya kudumu nchini wanaorudi kutoka nchi za nje watawekwa katika mazingira yafananayo na karantini kwa muda wiki mbili.
- Kwa sasa hivi wananchi na watu wanaoishi Ufini, wanapaswa kuepukana kusafiri nje nchi. Wananchi na watu wanaoishi Ufini wanaruhusiwa kurudi Ufini. Wasafiri wa nchi za nje wanaruhusiwa kutoka nje ya nchi.

Harakati zilizotajwa hapo juu zitaweza kuendelea au mabadiliko yanaweza kutokea. Maarifa haya yatafuliwa panapohitajika.